

MRENO ASHTAKIWA NA TANGANYIKA UNO

DAR ES SALAAM, Alhamisi.

Mwafika
SERIKALI ya Tanganyika leo imeishtaki Ureno katika Umoja wa Mataifa (UNO) kwa sababu ya ille tukio la Wareno wawili ambao juzi waliingiza nchini Tanganyika kutoka Msumbiji, ndege ya kivita ya Kireno yenye silaha.

Baada ya ndege hiyo kutua kwenye uwanja wa Dar es Salaam, Wareno hao wawili wametiwa nguvuni ili wapate kunojwa na hiyo ndege yao imezuiwa na Serikali.

Mpaka hivi leo mashtaka hayo yaliipopolekwa UNO, Serikali najasema Wareno hao pamoja na ndege na silaha zao watafanyiwa nini. Lakini msemaji wa Wizara ya Usalama nchini amemwambia ripota wetu kuwa uchunguzi kuhusu tukio hilo bado unaendeshwa.

Taarifa ya Serikali ya Tanganyika iliyopelekwa kwa Katibu Mkuu wa UNO, Bw. U Thant inasema: "Jioni ya Machi 12, 1963 ndege ya Kireno yenye silaha iliingia katika

nchi ya Tanganyika kwa njia ya uhalifu.

"Tukio hilo baya la kushtua ni miongoni mwa rekodi ndetu ya Kireno katika historia yake ya kutokujali sheria za ulimwengu.

"Lawama rasmi inatengenezwa ili ipelekwe kwa Serikali ya Salazar, ikianzamana na onyo kwamba Tanganyika itachukua hatua zitakazolazimika ili kuzura pasitokee tena kendo cha uhalifu."

Katibu wa wizara ya mambo ya nchi za nje, Dr. V. Kyaruzi amesema kuwa taarifa hiyo ya Serikali kwa UNO, kwa hali yoyote haina maana kwamba Tanganyika imepuuza kendo cha Wareno wawili hao. "Yaani ndege ya kivita kutua Dar es Salaam bila ruhusa, kwa hiyo sheria ya ulimwengu."

Ameongeza kusema: "Taarifa hiyo kwa UNO na lawama kwa Ureno ni kwa sababu ya tukio hilo. Ikiwa wakati wa uchunguzi, mambo yatagunduliwa zaidi, hatua ya kufaa itachukuliwa."

Deputy Information
Secretary, Frelimo

Ats...
D. ...
Frelimo